

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

**KUELEKEA MWISHO WA AWAMU YA KWANZA YA KUTUMA
MAOMBI YA UDAHILI KATIKA VYUO VYA ELIMU YA JUU KWA
MWAKA WA MASOMO 2018/19**

1.0 Utangulizi

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kuutangazia na kuukumbusha umma wa Watanzania, Taasisi za Elimu ya Juu na Wadau wote wa Elimu ya juu kwamba, **dirisha la maombi ya kujiunga na masomo ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu hapa nchini linatarajiwa kufungwa rasmi tarehe 15/08/2018. Mtakumbuka kwamba dirisha hili lilifunguliwa rasmi tarehe 20/07/2018 kwa awamu ya kwanza.**

2.0 Utaratibu wa Maombi ya Udahili kwa Mwaka wa Masomo 2018/19

2.1 Makundi ya Waombaji

Udahili unahusu makundi makubwa matatu ya waombaji:

a) Kidato cha Sita

b) Wenye sifa linganifu (Equivalent applicants) - Stashahada
(Diploma), FTC, NTA6

c) Waombaji wenye vyeti toka nje ya nchi vyenye sifa linganifu

2.2 Utaratibu wa kuomba udahili

a) Waombaji wote wa udahili wanapaswa kutuma maombi yao moja kwa moja kwenye vyuo wanavyopenda na kuchagua programu za masomo wanazopenda. Tume imetoa mwongozo wa programu zilizoidhinishwa kudahili pamoja na vigezo vya udahili vinavyotakiwa kwa kila programu ya masomo (*List of Approved Undergraduate Degree Programmes to admit students in 2018/2019 Academic Year*). Mwongozo huo unapatikana kwenye tovuti ya Tume [**www.tcu.go.tz**](http://www.tcu.go.tz).

b) Maelekezo mahsusi kuhusu jinsi ya kuomba programu ya masomo hutolewa na vyuo husika.

2.3 Vigezo na Sifa za Waombaji

Waombaji wote wanapaswa kukidhi vigezo na sifa stahiki za udahili zilizoidhinishwa na Tume kama ilivyobainishwa katika ***Jedwali Na. 1 na Jedwali Na. 2***

2.4 Mambo Muhimu ya Kuzingatia

2.4.1: Wakati wa kutuma maombi

a) Waombaji wote wanasisitizwa kusoma mwongozo wa programu zilizoidhinishwa kudahili pamoja na vigezo vya udahili vinavyotakiwa kwa kila programu ya masomo kabla ya kuanza kutuma maombi yoyote ya udahili.

b) Waombaji wanashauriwa kuwasiliana na vyuo wanavyopenda kwenda kusoma ili kupata taarifa za kina kuhusu programu za masomo wanazotarajia kuomba udahili kwa lengo la kujiridhisha kabla ya kutuma maombi.

- c) Waombaji wenye vyeti vya nje ya nchi ni lazima wawasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili kupata ithibati ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kuomba udahili.
- d) Vyuho Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu zinazodahili wanafunzi wa shahada wameelekezwa kuwa na mifumo ya kielekroniki kwa ajili ya kupokea, kuchakata, na kudahili wanafunzi ili kurahisisha zoezi la udahili.
- e) Waombaji wote, Vyuho Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu wanakumbushwa na kuhimizwa kuzingatia kalenda ya udahili iliyoidhinishwa na Tume (**Jedwali Na. 3**) ili kuepusha usumbufu usio wa lazima. Waombaji wote wanahimizwa kutumia muda huu uliobaki kukamilisha maombi yao.

2.4.2: Baada ya kufungwa rasmi kwa dirisha la maombi

- a) Baada ya kuufungwa rasmi kwa dirisha la udahili Vyuho vitaanza kuchakata majina ya waombaji kulingana na vigezo vya udahili vilivyowekwa kwa kila programu ya masomo.

b) Baada ya kukamilisha kuchakata majina ya waombaji, orodha ya waombaji itaidhinishwa na Seneti au Bodi za Kitaaluma za vyuo husika kabla ya kuwasilisha TCU.

c) Orodha ya waombaji walioidhinishwa na Seneti au Bodi za Kitaaluma itawasilishwa TCU kwa ajili ya kuhakiki kama waombaji waliochaguliwa na vyuo husika wana sifa stahiki na wanakidhi vigezo vya kujiunga na programu husika za masomo.

d) Baada ya TCU kuchambua orodha ya waombaji iliyowasilishwa na vyuo, itawasilisha vyuoni orodha inayobainisha waombaji wenye sifa ambao wanastahili kudahiliwa na vyuo.

- e) Kwa waombaji ambao watabainika kuwa wamechaguliwa katika programu za masomo zaidi ya moja, au kuchaguliwa katika chuo zaidi ya kimoja, watatumiwa ujumbe mfupi wa simu (SMS) wenye namba maalum ya siri ambayo wataitumia kuthibitisha chuo wanachotaka/wanachopenda kwenda kusoma. Tume inasisitiza kuwa namba hii ya siri itakuwa ni siri ya mwombaji na anatakiwa kuitoa pale tu anapotaka kuthibitisha chuo anachotaka kusoma. Tume itatoa muda maalum kwa waombaji kuthibitisha chuo au programu ya masomo anayopenda.
- f) Baada ya kukamilika kwa zoezi la udahili vyuo vitatakiwa kuchapisha orodha ya waombaji waliodahiliwa na kuwaarifu rasmi kuwa wamedahiliwa katika vyuo hivyo.

Imetolewa na

Katibu Mtendaji

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

14 Agosti 2018

Table 1: Minimum Admission Entry Qualifications for 2018/2019 Admission Cycle

NO.	CATEGORY OF APPLICANTS	MINIMUM ADMISSION ENTRY QUALIFICATIONS
1	Completed A-Level studies before 2014	Two principal passes with a total of 4.0 points from Two Subjects defining the admission into the respective programme (where A = 5; B = 4; C= 3; D = 2; E = 1).
2	Completed A-Level studies in 2014 and 2015	Two principal passes (C and above) with a total of 4.0 points from Two Subjects defining the admission into the respective programme (where A = 5; B+ = 4; B = 3; C= 2; D = 1). Grade 'D' is not considered as a principal pass in this category.
3	Completed A – Level studies from 2016	Two principal passes with a total of 4.0 points from Two Subjects defining the admission into the respective programme (where A = 5; B = 4; C= 3; D = 2; E = 1).
4	Equivalent applicants	<p>At least four O'-Level passes (Ds and above) or NVA Level III with less than four O'-Level passes or equivalent foreign qualifications as established by either NECTA or VETA; AND</p> <p>i) At least a GPA of 3.0 for Ordinary Diploma (NTA Level 6); OR</p> <p>ii) Average of C for Full Technician Certificate (FTC) (where A=5, B=4, C=3, and D=2 points); OR</p> <p>iii) Average of 'B' Grade for Diploma in Teacher Education; OR</p> <p>iv) Average of 'B' Grade for Health-related awards such as Clinical Medicine and others; OR</p> <p>v) A Distinction for unclassified diplomas and certificates.</p> <p>vi) Upper Second Class for classified non-NTA diplomas.</p>

Table 2: Admission Requirements for Direct Entrants and Equivalent Entrants for health related programmes

A: Direct Entrants		
SN	DEGREE PROGRAMME	ENTRY REQUIREMENTS
1	Doctor of Medicine (MD/MBBS)	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 8 points. Whereby one must have at least C grade in Chemistry and Biology and at least D grade in Physics .
2	Doctor of Dental Surgery (DDS)	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 8 points. Whereby one must have at least C grade in Chemistry and Biology and at least D grade in Physics .
3	Bachelor of Pharmacy (BPharm)	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 8 points. Whereby one must have at least C grade in Chemistry and Biology and at least D grade in Physics .
4	Bachelor of Medical Laboratory Sciences (BMLS)	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 6 points. Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics .
5	Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology (BSc RTT)	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 6 points. Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics .
6	Bachelor of Science in Prosthetic and Orthotics (BSc PO)	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 6 points. Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics .
7	Bachelor of Science in	Three principal passes in Chemistry, Biology

A: Direct Entrants		
SN	DEGREE PROGRAMME	ENTRY REQUIREMENTS
	Nursing (BScN)	and either Physics or Mathematics or Nutrition with a minimum of 6 points . Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics or Mathematics or Nutrition .
8	Bachelor of Science in Environmental Health Sciences (BSc EHS)	Three principal passes in Chemistry, Biology and either Physics or Mathematics or Nutrition or Geography or Agriculture with a minimum of 6 points . Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics or Mathematics or Nutrition or Geography or Agriculture .
9	Bachelor of Medical Laboratory Sciences in Clinical Chemistry, Bachelor of Medical Laboratory Sciences in Hematology and Blood Transfusion, Bachelor of Medical Laboratory Sciences in Histotechnology, Bachelor of Medical Laboratory Science in Microbiology and Immunology, Bachelor of Medical Laboratory Sciences in Parasitology and Medical Entomology and Bachelor of Medical Laboratory Sciences General	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 6 points . Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics .
10	Bachelor of Sciences in Health Laboratory and Bachelor of Science in	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 6 points . Whereby one must have at least C grade in Chemistry and at least D grade in Biology and E grade in Physics .

A: Direct Entrants		
SN	DEGREE PROGRAMME	ENTRY REQUIREMENTS
	Physiotherapy	
11	Bachelor of Science in Optometry	Three principal passes in Physics, Chemistry, and Biology with minimum entry of 6 points. Whereby one must have at least C grade in Physics and at least D grade in Biology and E grade in Chemistry/Mathematics
B: Equivalent Entrants		
<p>All equivalent applicants may apply for above programmes if they meet the requirements stated below:</p> <p>i. Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with at least Five (5) passes including two credit passes in Chemistry and Biology and a D grade in Physics PLUS appropriate Diploma or Advanced Diploma with an average of “B+” or GPA of 3.5</p> <p>OR</p> <p>ii. BSc (lower second) majoring in Physics/Mathematics, Chemistry, Biology /Zoology.</p>		

Table 3: Admission Almanac for 2018/2019 Admission Cycle.

SN	Activity	Responsible	Date
1.	Opening applications window for applicants who completed F6 and Diploma in previous years.	Students and HLIs	18th June 2018
2.	Opening application window for applicants who completed F6 and Diploma in 2018.	Students and HLIs	20th July 2018
3.	Deadline for 1st round of applications.	Students and HLIs	15th August, 2018
4.	Second Round applications.	Students & HLIs	3rd – 7th Sept 2018
5.	Third Round of applications.	Students & HLIs	19th -21st Sept 2018
6.	The Earliest date for opening of institutions.	HLIs	29th October 2018
7.	Deadline for submitting all students registered in 2018/19 Academic year.	HLIs	26th November 2018